

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Anuwani ya Simu "Hazina" DODOMA
Simu Nambari: +255 - 26 - 2160000,
Nukushi: +255 26 2963109
Barua pepe ps@hazina.go.tz
Tovuti : www.mof.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Hazina,
S.L.P 2802,
40468 DODOMA.

Unapojibu tafadhalu taja:
Kumb. Na.FB.41./457/01/145

25 Januari, 2022

Kwa wadau wote wa Ununuzi wa Umma na Ugavi

**YAH: MWALIKO WA KUSHIRIKI TUKIO LA WIKI YA UNUNUZI WA
UMMA ITAKAYOFANYIKA KUANZIA TAREHE
23 HADI 25 FEBRUARI, 2022 JIJINI ARUSHA**

Tafadhalu rejea somo tajwa hapo juu.

2. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Taasisi zinazosimamia sekta ya Ununuzi wa Umma na Ugavi yaani; Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma (PPAA), Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), imepanga kuendesha Wiki ya Ununuzi wa Umma kuanzia tarehe 23 hadi 25 Februari, 2022, Katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano (AICC) Jijini Arusha, ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Philip Isidory Mpango**.


3. Tukio hilo lenye Kaulimbiu "**Matumizi ya Teknolojia katika Kuboresha Ununuzi wa Umma**" ni fursa kwa Wadau wa Ununuzi wa Umma na Ugavi kupata elimu, kubadilishana uzoefu na mawazo kuhusu utekelezaji wa shughuli za ununuzi. Pamoja na mambo mengine, katika Wiki hiyo kutakuwa na Kongamano litakalohudhuriwa na Wadau mbalimbali wa sekta ya ununuzi wa umma na ugavi kwa lengo la kujadili masuala ya ununuzi na ugavi, changamoto na namna ya kuzikabili. Sambamba na Kongamano hilo, kutakuwa na maonesho ya siku tatu ambapo Wadhamini kutoka sekta za umma na binafsi watapata fursa ya kuonesha bidhaa na huduma zao kwa wadau na Umma kwa ujumla.

4. Washiriki katika tukio la Wiki ya Ununuzi wa Umma ni pamoja na Wajumbe wa Bodi na Wakuu wa Taasisi za Umma, Wajumbe wa Bodi za Zabuni, wataalam wa Ununuzi na Ugavi kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi,

Watumishi wa Idara za Sheria, Ukaguzi wa Ndani na Idara Tumizi. Washiriki wengine ni wazabuni, watoa huduma na wakandarasi, pamoja na washauri elekezi na wanafunzi wa masomo ya ununuvi na ugavi katika taasisi za elimu ya juu, na wawakilishi kutoka Asasi za Kiraia.

5. Hivyo, kwa barua hii, ninapenda kuwaalika wadau wote wa ununuvi wa umma kushiriki katika tukio hili la Wiki ya Ununuvi wa Umma ambalo litakuwa ni tukio la kwanza kabisa kufanyika katika historia ya Sekta ya Ununuvi wa Umma na Ugavi nchini.
6. Ada ya ushiriki kwa kila mshiriki **ni Shilingi 500,000/=** ambayo itahusisha gharama za chakula wakati wa Kongamano na huduma nyingine za kumuwezesha mshiriki kuchukua taarifa muhimu katika tukio hilo. Mshiriki anapaswa kuwezeshw na taasisi yake fedha za kujikimu na gharama nyingine. Malipo ya ushiriki yafanyike kupitia **Akaunti Namba 20110031672 - PPRA TANePS**, Benki ya NMB au kupitia **Akaunti Namba 0150500820100 - PPRA GePG Collection Account**, Benki ya CRDB. Mwisho wa kulipa ada ya ushiriki wa tukio hilo ni tarehe 15 Februari, 2022.
7. Kwa taarifa au ufanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Bw. Mcharo Mrutu kupitia namba **0754201032**, barua pepe: mcharo.mrutu@ppra.go.tz au Bi. Hilda Segele kupitia namba ya simu **0785 455034**, barua pepe: hilda.segele@hazina.go.tz.

Wako katika ujenzi wa Taifa,



Emmanuel M. Tutuba
KATIBU MKUU NA
MLIPAJI MKUU WA SERIKALI